

# Kikosi Kazi Kinachojumuisha Sekta Mbalimbali: Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Watoto

ACHA! Ukatili kwa watoto
WALINDE

# Kikosi kazi kinachojumuisha Sekta Mbalimbali: Mpango wa Taifa wa kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Watoto

# Usuli

Ripoti ya Dunia ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Ukatili dhidi ya Watoto ambayo ilifanyika kuanzia mwaka 2001 na kukamilika mwaka 2006, ilikuwa ndiyo utafiti wa kwanza na wa kina wa dunia juu ya aina zote za ukatili dhidi ya watoto. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchunguza, kutoa taarifa na mapendekezo juu ya ukatili dhidi ya watoto unaofanyika katika hali mbalimbali ambazo watoto wanaishi —ikiwa ni pamoja na majumbani na kwenye familia, mashuleni, mfumo wa malezi na wa kutoa haki, sehemu za kazi na katika jamii.

Viwango vya ukatili vilivyoripotiwa katika hali zote vilikuwa ni vya juu sana na vya kutisha: Sehemu zilizodhaniwa kuwa ni salama zilionyeshwa kuwa hazikuwa salama. Aina ya ukatili ulioripotiwa na kuelezwa zilikuwa ni za kukera ikiwa ni pamoja na kupigwa, kuteswa, kudhalilishwa kijinsia na hata kuuwawa na walezi waliokabidhiwa watoto hao kwa matunzo ya kila siku. Ukatili dhidi ya watoto ulionekana kuwa ni jambo la kawaida lililokuwepo kila mahali.

Kutokana na ripoti hiyo, Umoja wa Mataifa na Serikali duniani kote waliweka ajenda ya dunia ili kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji na ukatili kwa kufuata Misingi ya Miongozo ifuatayo:

- Hakuna ukatili wa aina yoyote dhidi ya watoto uliohalalishwa. Ulinzi wanaopewa watoto usiwe mdogo kuliko wanaopewa watu wazima.
- Ukatili wa aina yoyote dhidi ya watoto unazuilika. Serikali lazima ziwekeze katika Sera zitakazotumia takwimu zenye kuonyesha hali halisi na mipango inayolenga kushughulikia mambo yanayosababisha kuwepo kwa ukatili dhidi ya watoto.
- Serikali zina wajibu wa msingi katika kutetea haki za watoto za kulindwa na kupatiwa huduma, na kusaidia familia ili ziwe na uwezo wa kuwapatia watoto malezi katika mazingira yaliyo salama.
- Serikali zina wajibu wa kuhakikisha unakuwepo uwajibikaji katika kila tukio la ukatili.
- Watoto, kuwa katika mazingira hatarishi na ya ukatili huendana na umri na uwezo wao wa kutathmini. Baadhi ya watoto huwa hatarini zaidi kwa sababu ya jinsia, kabila, asili ya kabila lao, ulemavu au hadhi yao kijamii.
- Watoto wana haki ya kutoa maoni, na maoni yao kutiliwa maanani wakati wa utekelezaji wa sera na mipango.

Ili kuhamasisha usambazaji wa matokeo ya ripoti na ufuatiliaji wa mapendekezo yake, Ripoti ya Dunia ilipendekeza uteuzi wa Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Bi. Marta Santos Pais, alianza kazi tarehe 1 Septemba, 2009. Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu ni mtetezi huru wa kimataifa katika juhudi za kuzuia na kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya watoto, kwa kuhamasisha vitendo na uungwaji mkono kisiasa ili kuendeleza juhudi za ajenda hii. Mwakilishi Maalum anatoa taarifa moja kwa moja kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, na hutoa taarifa kila mwaka kwa Baraza la Haki za Binadamu na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

# Utafiti juu ya Ukatili Dhidi ya Watoto nchini Tanzania na Kikosi Kazi kinachojumuisha Sekta mbalimbali 2008-2011



Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

# Utafiti juu ya Ukatili Dhidi ya Watoto nchini Tanzania na Kikosi Kazi kinachojumuisha Sekta mbalimbali 2008-2011

Wakati ripoti ya dunia ilitumika kuonyesha kuenea kwa ukatili, pia ilionyesha wazi kuwa sababu za unyanyasaji ni za kiutamaduni na hutokana na jamiii na hivyo kuzipa dhamana Serikali kuandaa mikakati mahususi ya kitaifa ya kushughulikia.



Mapendekezo yanayotokana na utafiti huu ni pamoja na kuanzisha na kutekeleza utaratibu mzuri wa kitaifa wa kukusanya data na kufanya utafiti, kuzitaka Serikali kuboresha ukusanyaji wa data na utaratibu wa upashanaji habari ili kuweza kuainisha makundi madogo yaliyo hatarini, kuwa na sera za kupashana habari na kuwa na mipango katika ngazi zote na kufuatilia maendeleo ya kulifikia lengo la kuzuia ukatili dhidi ya watoto.

Uswazi ilikuwa nchi ya kwanza kuitikia wito wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa kutekeleza na kuwasilisha *Utafiti wake wa Kitaifa juu ya Ukatili dhidi ya Watoto na Wanawake Vijana mwaka (2007),* ulikuwa utafiti wa kwanza wa aina yake uliolenga katika idadi ya watu na kupima kiwango cha ukatili dhidi ya watoto na hasa kwa wanawake. Tanzania ilikuwa ni nchi ya pili kufanya Utafiti wa Kitaifa juu ya *Ukatili Dhidi ya Watoto* katika Afrika lakini ilikwenda mbele kuliko ule utafiti wa Uswazi: Kwa mara ya kwanza katika Bara la Afrika aina zote za ukatili dhidi ya watoto (ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili) ulipimwa miongoni mwa wasichana na wavulana.

Mchakato wa kuandaa Utafiti juu ya Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania ulianza katikati ya mwaka 2008. Baada ya hapo Kikosi Kazi kinachojumuisha Sekta mbalimbali Tanzania kilianzishwa Septemba 2008, kikijumuisha wajumbe kutoka sekta za umma, asasi za kijamii na wadau wa maendeleo, ili kujenga dhana ya kufanya juhudi za pamoja sio tu kuongoza utafiti huu, bali pia utekelezaji wake na utoaji wa taarifa ya mwisho, na pia kusaidia katika kuongoza matokeo ya utafiti yatekelezwe kwa vitendo na kuzaa matunda yenye kuonekana ili kuendeleza mfumo wa kitaifa wa kuwalinda watoto.

Kuanzishwa kwa Kikosi Kazi kulikuwa na umuhimu mkubwa katika kuhakikisha kuwa mpango huu unamilikiwa na kusimamiwa kitaifa. Jingine ambalo ni la muhimu ni kuwa Kikosi Kazi kimevipa sauti vikundi vya jumuiya za kiraia ambazo zina jukumu muhimu la kushughulikia mahitaji ya jamii kule ambako huduma za kijamii zinazopaswa kutolewa na Serikali ya Tanzania hazijafika. Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto inafanya shughuli ya kuwa muandaaji na mratibu wa shughuli za Kikosi Kazi. Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto alichukua jukumu hili muhimu la uongozi mwezi Februari 2009 na kuuweka utafiti huu mikononi mwa serikali. Huko Zanzibar, Kikosi Kazi kama hiki kiliundwa mwezi Februari 2009 kikiongozwa wakati huu na Wizara ya Kazi, Vijana, Wanawake na Maendeleo ya Watoto. Uongozi madhubuti wa Serikali umekuwa ni mfano mzuri na utaendelea kuwa na jukumu muhimu katika kuimarisha mpango madhubuti wa kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto.

Wakati Vikosi Kazi vinavyojumuisha Sekta mbalimbali vikiwa vimeanzishwa Tanzania Bara na Zanzibar, kikundi cha utafiti kutoka Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Maradhi cha Atlanta, Marekani kiliwasili Dar es salaam kujadili, kutayarisha na kukubaliana juu ya mpango mzima wa utekelezaji wa Utafiti wa Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania (UUDWT) pamoja na muhtasari wa mpango wa utekelezaji, rasimu ya kidadisi na makisio ya mahitaji ya bajeti.

Wakati wote wa kipindi cha kuandaa mpango, wajumbe wa kikosi kazi kinachojumuisha sekta mbalimbali walishirikishwa katika kupitia mipango ya kazi, bajeti na madodoso, mpango wa utafiti na nyaraka za kuidhinisha maadili. Chuo Kikuu Shirikishi cha Afya na Sayansi ya Tiba cha Muhimbili kiliteuliwa kuwa mtafiti mshiriki wa hapa nchini na mtekelezaji mkuu wa utafiti – na kuziweka shughuli zote za utafiti chini ya chuo pekee nchini cha tiba na afya ya umma.

Ilipofikia mwezi Oktoba 2009, kikundi cha watafiti cha Kituo cha Kudhibiti Maradhi cha Atlanta na Chuo Kikuu Shirikishi cha Afya na Sayansi ya Tiba cha Muhimbili kwa pamoja walitoa mafunzo kwa kikundi cha watanzania wa kuongoza na kufanya mahojiano na majaribio ya ugani yalikamilika. Mwezi mmoja baadaye watoto na vijana 3,739 walihojiwa katika mikoa ishirini na moja (21) ya Tanzania na wilaya kumi (10) za Zanzibar. Ukusanyaji wa takwimu ulikamilika baada ya mwezi mmoja, mwishoni

wa mwaka 2009. Uchambuzi wa kina wa data ulifanyika kati ya Kituo cha Kudhibiti Maradhi kwa kushauriana na Chuo Kikuu Shirikishi cha Afya na Sayansi Tiba cha Muhimbili ambapo matokeo ya awali yaliwasilishwa kwenye Kikosi Kazi kinachojumuisha Sekta mbalimbali mwezi Julai 2010.

Matokeo ya mwisho yanayoonyeshwa hapa, yanadhihirisha kuwepo kwa changamoto kubwa kwa jamii ya watanzania, serikali na washirika wake wa kitaifa na kimataifa. Baada ya kueleza hayo, ushirikiano na msimamo wa Kikosi Kazi kinachojumuisha Sekta mbalimbali mpaka hivi sasa ni ishara kubwa yenye kutoa dalili ya kupatikana mpango wa taifa wenye kuwiana na ukubwa wa tatizo.

# Matokeo ya Utafiti juu ya Ukatili Dhidi ya Watoto: Kuenea kwa Ukatili Dhidi ya Watoto nchini Tanzania



Picha: UNICEF/Giacomo Pirozzi

# Matokeo ya Utafiti juu ya Ukatili Dhidi ya Watoto: Kuenea kwa Ukatili Dhidi ya Watoto nchini Tanzania



## Unyanyasaji wa kijinsia uliotokea utotoni

Unyanyasaji wa kijinsia una maana ya kitendo chochote kile, jaribio au tishio la kijinsia ambalo linasababisha au linaweza kusababisha madhara ya kimwili, kisaikolojia na ya kiakili. Matokeo yanaonyesha kuwa takriban mmoja kati ya wanawake watatu wenye umri kati ya miaka 13 hadi 24 nchini Tanzania walitoa taarifa ya kufikwa na angalau tukio moja la unyanyasaji wa kijinsia kabla ya kufikia umri wa miaka 18. Kwa wanaume wa rika hilo, zaidi ya mmoja miongoni mwa saba walitoa taarifa ya kufikwa na angalau tukio moja la unyanyasaji wa kijinsia kabla ya kufikia umri wa miaka 18. Lililo wazi kabisa ni kwamba, mwanamke mmoja kati ya ishirini alitoa taarifa ya kupatwa na tukio la ngono ya kulazimishwa kwa nguvu wakati wa utoto wake.

Zaidi ya mwanamke mmoja kati ya wanawake wanne waliohojiwa walitoa taarifa kuwa tendo lao la kwanza la ngono lilikuwa ni la kulazimishwa, ikiwa na maana kuwa walilazimishwa ama kwa kulaghaiwa, kushurutishwa, kutishwa na kwa kutumia nguvu kufanya ngono.

## Ukatili wa kimwili uliotokea utotoni

Jedwali 1: Ukatili wa kijinsia, Kimwili na kiakili uliotokea utotoni kwa wenye umri kati ya miaka 13-24 (Ripoti ya Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania 2009)




Ukatili ya kimwili dhidi ya watoto unaweza kuzuia maendeleo yao ya kimwili, ufahamu na kiakili. Utafiti umebainisha mara nyingi watoto walionyanyaswa kijinsia pia walipata madhara ya kimwili.

Takriban robo tatu ya wanawake na wanaume walitoa taarifa ya kutendewa ukatili wa kimwili kutoka kwa jamaa, mtu mwenye mamlaka (kama vile mwalimu[a]) au mwenzi wa karibu kabla ya kufikia umri wa miaka 18. Wingi ya unyanyasaji huu ulikuwa ni kwa kupigwa ngumi, kupigwa viboko au kupigwa mateke. Zaidi ya nusu ya wanawake na wanaume wenye umri kati ya miaka 13 hadi 17 walitoa taarifa kuwa wametendewa ukatili wa kimwili mwaka uliopita kutoka kwa jamaa, mtu mwenye mamlaka au mwenzi wa ndani.

## Ukatili wa kiakili uliotokea utotoni

Takriban robo ya wanawake na karibia wanaume 3 kati ya kila wanaume 10 wenye umri wa miaka 13 hadi 24 walitoa taarifa ya kufanyiwa ukatili wa kiakili na mtu mzima wakati wakiwa watoto. Na karibia

[a] Ni muhimu kubaini kuwa ukatili wa kimwili unapita kiwango kilichokubaliwa shuleni kama adhabu ya kuchapwa viboko. Sheria ya Kuchapwa Viboko ya 1979 ( iliyorekebishwa na Waraka wa Elimu namba 24 wa 2002) ulirekebisha na kuruhusu 'Viboko kwa makosa makubwa vitolewe na mkuu wa shule au mtu aliyekabidhiwa madaraka ya uongozi na mkuu wa shule, na visizidi viboko vinne'. Kwa Zanzibar Kanuni za Sheria ya Elimu za mwaka 1988 zinafafanua adhabu ya kuchapa viboko kuwa ni adhabu inayotolewa kwa kutumia fimbo nyepesi kwenye matako yaliyofunikwa mbele ya mtu mwingine ambaye ni miongoni mwa walimu wa shule.

mwanamke mmoja miongoni mwa wanawake ishirini na wanaume, wenye umri wa miaka 13 hadi 24 walitoa taarifa kuwa walitishiwa kutelekezwa na mtu mzima kabla ya kufikia umri wa miaka 18.

Kwa wanaume wa rika hilo, zaidi ya mmoja miongoni mwa saba walitoa taarifa ya kufikwa na angalau tukio moja la unyanyasaji wa kijinsia kabla ya kufikia umri wa miaka 18. Lililo wazi kabisa ni kwamba, mwanamke mmoja kati ya ishirini alitoa taarifa ya kupatwa na tukio la ngono ya kulazimishwa kwa nguvu wakati wa utoto wake. Takriban msichana 1 kati ya 10 alitoa taarifa kuwa mkosaji wa angalau tukio moja alikuwa mwalimu.

## Wahusika wa ukatili dhidi ya watoto

**Wahusika wa unyanyasaji wa kijinsia utotoni:** Mhusika anaweza kuwa mtu au kikundi cha watu ambao wanatenda moja kwa moja au wanaunga mkono kufanyika kwa ukatili au unyanyasaji dhidi ya mtu mwingine: mara nyingi, wahusika wanakuwa ni watu wenye uwezo wa dhahiri au wakudhaniwa, wa kufanya maamuzi na/au wenye madaraka na kwa hiyo wanaweza kuwa na udhibiti kwa waathiriwa.

Nchini Tanzania, majirani na watu wasio wanafamilia ndio ambao mara nyingi wanaotuhumiwa kuhusika na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya watoto wanawake. Takriban msichana 1 kati ya 10 walitoa taarifa kuwa mhusika mmoja wa tukio la ukatili alikuwa mwalimu. Watu wa karibu au wenzi wenye kujulikana na watu wasio wanafamilia ndio wahusika waliotuhumiwa mara nyingi kwa unyanyasaji dhidi ya watoto wanaume. Zaidi ya theluthi mbili ya wanawake walionyanyaswa kijinsia waliripoti kuwa mhusika wa angalau tukio moja alikuwa mkubwa kwa umri, wakati wanaume wengi waliopatwa na unyanyaswaji wa kijinsia waliripoti kuwa mhusika wa angalau tukio moja alikuwa ni wa umri sawa na yeye. Karibu theluthi mbili ya wanawake waliopatwa na unyanyaswaji wa kijinsia utotoni waliripoti kuwa waliathiriwa na mhusika aliyekuwa amemzidi umri kwa zaidi ya miaka 10.

**Wahusika wa ukatili wa kimwili kwa watoto:** Takriban wanawake na wanaume wawili kati ya watatu walifanyiwa ukatili wa kimwili na jamaa zaidi ya nusu walifanyiwa ukatili wa kimwili na walimu kabla ya kufikia umri wa miaka 18. Wanawake na wanaume wengi wenye umri wa miaka 13 hadi 24 walioripoti kufanyiwa ukatili wa kimwili kabla ya kufikia umri wa miaka 18 walifanyiwa ukatili na baba na mama zao.

**Wahusika wa ukatili wa kiakili kwa watoto:** Miongoni mwa wale waliofanyiwa ukatili wa kiakili kabla ya kufikia umri wa miaka 18, wanawake takriban 8 kati ya 10 na zaidi ya wanaume 6 kati ya 10 walitoa taarifa ya kunyanyaswa kwa kufanyiwa ukatili wa kiakili na ndugu.

Jedwali 2: Asilimia ya wasichana na wavulana chini ya umri wa miaka 18 waliotoa taarifa kwa mtu kuhusu ukatili wa kijinsia, waliotafuta huduma za ukatili dhidi ya jinsia na waliopata huduma hizo




* Makadilio sio kamili

## Tabia ya kutafuta msaada kwa watoto waliopatwa na Unyanyasaji wa Kijinsia nchini Tanzania

**Endapo Watanzania waliopatwa na unyanyasaji wa kijinsia kabla ya kufikia umri wa miaka 18 waliwahi kumwambia mtu yeyote kuhusu unyanyasaji huo:** Kwa wale waliopatwa na unyanyasaji wa kijinsia kabla ya kufikia umri wa miaka 18, takriban nusu ya waliokuwa na umri kati ya miaka 13 hadi 24 wanawake na wawili kati ya kila wanaume watatu wenye umri kati ya miaka 13 hadi 24 hawakumwambia mtu yeyote juu ya kunyanyaswa kwao.

**Sababu zilizotolewa na watoto hao kwanini hawakutoa taarifa juu ya unyanyaswaji huo wa kijinsia kwa maafisa wa ustawi wa jamii au polisi ni pamoja na mambo yanayohusiana:** na familia au jamii (k.m. hofu ya kutelekezwa au kutenganishwa, kutotaka kuzitia aibu familia zao), sababu za kibinafsi (k.m. hawakuona unyanyasaji huo kuwa ni tatizo, na imani kuwa hilo tatizo haliwahusu watu wengine, na muathiriwa kutaka kushughulika tatizo hilo mwenyewe), na kuhusu mhusika (k.m kutotaka kumtia mhusika matatani au vitisho kutoka kwake).

**Tabia ya utafutaji msaada miongoni mwa Watanzania waliopatwa na unyanyaswaji wa kijinsia kabla ya kufikia umri wa miaka 18:** Zaidi ya mwanamke 1 kati ya wanawake 5 na mwanamume 1 kati ya 10 waliopatwa na unyanyaswaji wa kijinsia kabla ya kufikia umri wa miaka 18 walitafuta huduma. Kwa jumla, ni zaidi kidogo ya mwanamke 1 kati ya 10 na mwanamume 1 kati ya 25 waliopatwa na unyanyaswaji wa kijinsia kabla ya miaka 18 waliripoti kuwa walipatiwa huduma.

Takriban mwanamke na mwanamume mmoja kati ya sita walionyanyaswa wa kijinsia utotoni walisema kuwa wangependa kupatiwa huduma za ziada, ikiwa ni pamoja na ushauri nasaha na msaada kutoka kwa polisi na maafisa wa ustawi wa jamiii.

**Vitendo vingi vya ukatili wa kijinsia hufanyika mchana kweupe:** Vitendo vingi vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wavulana na wasichana vilifanyika kati ya adhuhuri na saa 2 usiku. Angalau tendo moja la ukatili wa kijinsia lilifanyika kati ya adhuhuri na saa 11 jioni. Hii ni sawa na asilimia 43.4 kwa wasichana na asilimia 35.4 kwa wavulana. Zaidi ya theluthi moja ya wasichana na wavulana walisema kuwa walifanyiwa ukatili wa kijinsia kati ya saa 11 jioni na saa 2 usiku. Wavulana na wasichana wachache sana walisema kuwa walifanyiwa ukatili wa kijinsia kati ya usiku wa manane na saa 1 asubuhi.

**Uhusiano kati ya ukatili wa kijinsia na VVU na UKIMWI:** Utafiti pia uliangalia uhusiano kati ya ukatili wa kijinsia, ukimwi na tabia hatarishi. Ngono ya kulazimishwa au kushurutishwa inaweza kusababisha maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi, na ukatili, au vitisho humfanya muathirika ashindwe kutumia kinga. Matumizi ya kondomu miongoni mwa wanaume na wanawake waliofanyiwa ukatili wa kijinsia utotoni ni kidogo sana ikilinganishwa na wale ambao hawakufanyiwa ukatili huo. Kuna uwezekano mkubwa kwa wanaume na wanawake wa Tanzania waliofanyiwa ukatili wa kijinsia kuwa na wapenzi wengi kuliko wale ambao hawakufanyiwa ukatili huo. Biashara ya ngono inafanywa zaidi na wasichana waliofanyiwa ukatili wa kijinsia utotoni kuliko wale ambao hawakufanyiwa ukatili huo.

**Ukatili wa kijinsia na kimwili huathiri afya ya wanawake:** Wanawake wa Tanzania wanaofanyiwa ukatili wa kijinsia wana uwezekano mkubwa wa kupatwa na msongo wa mawazo, kupata magonjwa ya zinaa na kujiingiza katika unywaji pombe ikilinganishwa na wale ambao hawakufanyiwa ukatili huo. Hali kadhalika, wanawake wa Tanzania waliofanyiwa ukatili wa kupigwa wana uwezekano mkubwa wa kuathirika kiafya, kuwa na wasiwasi, na kuwa na mawazo ya kujiua.

**Gharama ya ukatili dhidi ya watoto:** Tafiti nyingine zimeonyesha gharama ya afya ya binadamu, kijamii na kiuchumi ya kutokutekeleza haki ya ulinzi kwa watoto, ni kubwa na haikubaliki. Gharama zilizo wazi ni za matibabu, sheria, huduma za ustawi wa jamii na huduma mbadala za matunzo. Gharama zisizo wazi ni pamoja na kupata ulemavu wa kudumu, gharama za magonjwa ya akili au matatizo mengine yanayodidimiza maisha, kukatiza masomo au uwezo wa kuwa mtu mzima atakeyeweza kuchangia kujenga uchumi. Pia gharama zinahusiana na makosa ya uhalifu yanayofanywa na watoto ambao walifanyiwa ukatili utotoni.

## Kutoka utafiti kwenda kwenye vitendo: Mpango wa sekta kwa sekta wa Kikosi Kazi kinachojumuisha sekta mbalimbali



Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

# Kutoka utafiti kwenda kwenye vitendo: Mpango wa sekta kwa sekta wa Kikosi Kazi kinachojumuisha sekta mbalimbali

Utafiti wa Tanzania umeonyesha wazi na kutia huzuni kuwa ukatili dhidi ya wasichana na wavulana ni tishio kubwa kwa afya na ustawi wa taifa. Yaliyoonekana Tanzania yanafanana sana na yale yaliyoonekana Uswazi miaka miwili iliyopita na kutoa viashiria vya kwanza ambavyo wataalam wanadhani utakuwa ndio mwelekeo wa dunia nzima. Matokeo muhimu zaidi ya utafiti huu ni ushahidi uliojitokeza ambao utahimiza hatua zinazohitaji kuchukuliwa kushughulikia ukatili dhidi ya watoto.

Jedwali Na 3. Mfumo Madhubuti wa Ulinzi wa Watoto. Ulinzi na Huduma za Kuzuia Ukatili Dhidi wa Watoto.




## Nchini Tanzania, ushahidi uko wazi na jibu ni wito wa kuwepo kwa juhudi za kitaifa

Kikosi Kazi kina jukumu la kuwa chachu katika kuhakikisha kuwa sekta zote husika ziko tayari na zinaweza kutoa itifaki na huduma zilizo rafiki kwa watoto ili kuhakikisha kuwa watoto walioathiriwa wanapata tiba na kutunzwa kwa kupatiwa huduma zote zinazohitajika ili kurejea katika maisha ya afya njema.

La umuhimu ni kwamba sekta hizo hizo zinahitaji kwenda mbele zaidi ya kutoa huduma na kufanya kazi pamoja na jamii kila mahali katika Jamhuri yote, kuwashirikisha viongozi, wadau, wenye madaraka ya maamuzi, na vijana wenyewe katika wito wa jumla wa kutovumilia kabisa ukatili wa namna yoyote ile: wa kimwili, kihisia au kijinsia.

## Haki na Polisi

Kufuata sheria na kuzitekeleza kwa kupitia kikosi cha polisi wanaoelewa vyema ni muhimu ili kutoa haki na ulinzi kwa watoto wote nchini Tanzania. Kupitishwa kwa Sheria ya Mtoto Na 21 (2009) kumeweka kiwango kwa ajili ya kuwalinda watoto, kiwango kilicho juu kama kingine chochote katika bara hili. Kanuni za Sheria ya Mtoto Na 21 (2009), zinazoandaliwa hivi sasa, zitaweka taratibu zinazohusu sekta mbalimbali zitakazombana mtu kisheria na zitaweka viwango kwa ajili ya kuainisha, kupeleka mahakamani na kushughulikia kesi za unyanyasaji wa mtoto, na majukumu na wajibu wa wahusika wote na uwezo wa watendaji.

Mara nyingi Polisi ndio wanakuwa wa kwanza kufikiwa na mahali pekee pa mawasiliano kwa waathiriwa, kwa kupitia idadi inayozidi kukua ya madawati ya Jinsia na Watoto nchini Tanzania. Hapo ndipo pamoja na matibabu ya dharura, kesi za unyanyasaji na ukatili zinaporipotiwa na baadaye kupelekwa mbele kwa hatua za kisheria. Polisi wana jukumu la msingi katika kuhakikisha watoto waathirika wa ukatili wanapata huduma za sheria kwa haraka, na kwa umakini kwa njia ambayo itazuia wasinyanyaswe na wakosaji wanawajibishwa kwa makosa waliyotenda. Maafisa wa polisi watahitaji mafunzo juu ya namna ya kushughulikia mahojiano na watoto waathiriwa na upelelezi. Ikiwa kama sehemu ya utaratibu wa kutambua, kuandaa mashtaka na kufuatilia kesi za unyanyaswaji wa watoto, mafisa wa polisi wanatakiwa kuhakikisha kunakuwepo ushirikiano na sekta nyingine ili kujenga mfumo wa kwanza wa

kuzuia na kukabiliana na matatizo yote ya ulinzi wa watoto, bila kumwacha nyuma mvulana au msichana yeyote wa Kitanzania. Mafunzo ya mwingiliano ya sekta mbalimbali yatasaidia kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya polisi, ustawi wa jamii, sheria na afya.

**Hatua zinazopendekezwa:**

- Kuchangia na kuunga mkono mchakato wa kutunga kanuni na taratibu kuhusu Sheria ya Mtoto Na 21 (2009) zitakazofafanua majukumu na wajibu wa sekta zote katika kutoa huduma ndani ya Mfumo wa Taifa wa Kuwalinda Watoto nchini Tanzania.
- Kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto —ambayo ina jukumu la kuratibu Sheria ya Mtoto Na 21 (2009) —katika kuandaa mpango wa taifa wa utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Na 21 (2009).
- Kutuo ushauri kuhusu mafunzo ya vyuoni na ya kazini yanayohusu utekelezaji wa Sheria ya Mtoto katika sekta zote zilizopewa jukumu la kisheria kuwalinda watoto.
- Kujenga uwezo wa rasilimali watu na vifaa kwa Kikosi cha Polisi cha Tanzania ili kuweza kutoa huduma za kutosha na za kirafiki kupitia Madawati ya Jinsia na Watoto
- Kuhakikisha uchunguzi wa polisi kuhusu kesi za ukatili kwa watoto zinafuata Miongozo ya Utafiti wa makosa ya ukatili dhidi ya watoto ambayo yanakidhi mahitaji ya watoto waathirika.
- Kuendeleza mpango wa majaribio wa Polisi Jamii na kipindi cha 'Usalama wetu kwanza' mashuleni kuenea nchi nzima

## Afya

Kupata huduma ya dharura ya matibabu isiyo na vipingamizi na matunzo yanayofuata, ndiyo huduma muhimu ya haraka inayotolewa kwa watoto ambao ni waathiriwa wa udhalilishaji. Kwa kiasi kikubwa, watoto hawapati huduma ipasavyo katika mfumo uliolenga kuwahudumia watu wazima na hivyo itifaki ni lazima ziandaliwe kwa taratibu za kumjali mtoto. Waathiriwa wote wa udhalilishaji wa kijinsia wanahitaji matibabu ya kinga kwa Magonjwa ya zinaa yenye kuambukiza ikiwa ni pamoja na yale ya kinga baada ya ngono ili kuwalinda dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI na dawa za dharura za kuzuia mimba kwa wasichana ili kuwalinda na mimba zisizotakiwa. Matunzo yanayofuata baada ya matibabu ya dharura ndiyo yatakayo onyesha uwezo wa muathiriwa kuishi muda mrefu hasa katika sehemu ya ushauri nasaa wa kisaikolojia na kijamii. Hivi sasa, Sera ya Ukatili yenye Kulenga Jinsia na Mwongozo Madhubuti wa Kusimamia Ukatili wa Kijinsia zinaandaliwa kwa makubaliano kuwa miongozo na huduma hizi lazima zitambue mahitaji mahasusi ya watoto. Mchakato wa kuandaa sera za kitaifa na miongozo unaweza kuhamasisha kuwepo kwa ushirikiano wa sekta mbalimbali.

Mafanikio ya kudumu ya mtazamo wa kweli wa pamoja unahitaji ushiriki kamili wa wana jamii wote. Miundo inayojumuisha uangalizi kwenye nyaja mbalimbali imeonekana kuwa inafaa. Huduma jumuishi zenye kulenga ndani na nje ya mfumo wa afya zinaweza kujenga ubora na mfumo mzuri wa kupata huduma ya afya. Swala hili linaambatana na uwezo wa mtoa huduma hizi ambao unabaki kuwa kipingamizi kikubwa katika kujenga ubora wa huduma zilizo na nyanja nyingi. Kwa hali ilivyo sasa madaktari hukusanya ushahidi unaohitajiwa mahakama tu, hali ambayo inadhoofisha nafasi ya muathiriwa kupata maangalizi ya kiafya na haki – kupanua dhamana hii kwa watalaamu wengine wa afya wenye sifa ya huduma za uangalizi wa kiafya inapaswa kufikiriwa. Watoaji wa huduma hizi lazima wapatiwe mafunzo ya kila wakati ya idara mbalimbali za afya na taaluma nyingine Kwa mfano, ujuzi unaohitajika katika kutoa huduma ya UKIMWI na Ukatili wa Kijinsia unatofautiana, na kwa maana hiyo, watoa huduma kwenye nyanja zote mbili wapaswa kujua njia bora za kutoa huduma na kuwalinda watoto. Pia, tabia nyingi hatarishi ziko kote kwenye UKIMWI na ukatili wa kijinsia. Ngono ya kulazimishwa utotoni au wakati wa ujana, imeonyesha kuchangia kujenga tabia ya kufanya ngono bila kinga, kuwa na wapenzi wengi, kujihusisha na biashara ya ngono na kutumia madawa ya kulevya – tabia zote hizi hatarishi zinaweza kuchangia ongezeko la maambukizi ya UKIMWI.

Hali kadhalika, karibia asilimia 7 ya wanawake, wenye umri kati ya miaka 13 hadi 24 ambao walikuwa wajawazito, walitoa taarifa kuwa tukio moja la uja uzito lilisababishwa na ukatili wa kijinsia. Huduma za afya kwa watoto na vijana zinapaswa kuwa na wigo pana.

**Hatua zinazopendekezwa:**

- Kuhakikisha kuwa maswala ya afya ya kiakili na kimwili ya mtoto yanayohusiana na kukabilina na ukatili, matunzo na matibabu yanaingizwa katika miongozo na taratibu za kazi zilizoandaliwa kwa muktadha wa ukatili unaolenga jinsia katika sekta ya afya.

- Kushajiisha kuwepo kwa kiungo madhubuti kati ya ukatili wa kijinsia, afya ya uzazi kwa vijana na uzuiaji wa VVU/ UKIMWI, huduma za matunzo na matibabu kwa kutilia mkazo zaidi juu ya uhusiano kati ya Ukatili wa kijinsia, mimba za ututoni na VVU/UKIMWI.
- Kuinua mwamko wa jamii juu ya ukatili dhidi ya watoto kuwa ni suala muhimu la afya ya jamii na kujumuisha njia za kujadili kwa uwazi, njia za kuzuia na kukabiliana na ukatili.
- Kujenga mfumo wa kuwajengea uwezo watoaji huduma za afya kukabiliana na udhalilishwaji wa watoto kijinsia pamoja na udhalilishwaji wa kimwili na kijinsia kwa kuwapatia mafunzo wakiwa vyuoni na kazini ikiwa kama sehemu ya kuboresha matibabu na matunzo ya afya za watoto.

## Elimu

Watoto hutumia muda wa saa 12 kila siku wakiwa shuleni na mazingira yake lakini utafiti umebainisha kuwa shule nyingi Tanzania sio salama.

Hatua kadhaa inabidi zichukuliwe katika sekta ya elimu kuhakikisha shule zote zinatokomeza ukatili na hatua za nidhamu zinafuatwa kwa walimu watakotenda ukatili kwa watoto.

Kanuni za maadili kwa ajili ya mashule zilizopo hivi sasa (pamoja na maadili ya kitaaluma na mwenendo wa walimu) zina haja ya kuangaliwa upya na kuongeza viwango vya ulinzi wa watoto. Adhabu ya kuchapa viboko inahitaji kuangaliwa upya na miongozo kwa walimu juu ya nidhamu mbadala. Ulinzi wa watoto na njia za kufundisha zisizo na ukatili zinahitajika ziwe ni sehemu ya mafunzo kwenye vyuo vya walimu na mafunzo kazini. Uhamasishaji wa ulinzi wa watoto mashuleni na katika jamii kwa ujumla haina budi kutiliwa mkazo kwa kuimarisha uhusiano wa wazazi, watoto na viongozi wa jamii katika uratibu wa shule. Wazazi wanahitaji kuhamasishwa waelewe mipaka ya nidhamu, na mchakato wa kuelimisha suala la haki za mtoto na kuheshimu mawazo yao uzingatie mbinu zitakazowajengea wazazi uwezo.

**Hatua zinazopendekezwa:**

- Kuhakikisha kuwa Kanuni za Maadili ya Walimu na huduma ya Ushauri nasaa kwa wanafunzi vinatekelezwa katika shule zote.
- Kuunga mkono mpango madhubuti wa utekelezaji wa pamoja na Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu juu ya njia bora ya kitaifa ya kutekeleza yatokanayo na Ripoti ya Ukatili dhidi ya Watoto, pamoja na, uandaaji wa elimu ya haki za mtoto na haki ya kulindwa, ambayo itajumuisha mafunzo ya majukumu kuendana na Sheria ya Mtoto katika kutoa taarifa ya kesi za ukatili, na yatakuwa ni sehemu muhimu na ya lazima katika mafunzo ya vyuoni na mafunzo ya kazini.
- Kuandaa Kitabu cha Ulinzi kwa watoto na kuwashirikisha baadhi ya Wakurugenzi wa Elimu wa Wilaya kuvifanyia majaribio vitabu hivyo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji na kuingiza mfumo wa kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto ili wanafunzi waathiriwa waweza kuzifikia huduma zote zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria.
- Kuimarisha juhudi za kuzuia ukatili dhidi ya watoto kwa kuwashirikisha watoto mashuleni na wazazi wao katika ngazi za jamii pamoja na kuweka utaratibu wa uwajibikaji kati ya walimu na wazazi katika kupambana na ukatili dhidi ya watoto.
- Kuanzisha utaratibu wa kutoa taarifa, ufuatiliaji na kuratibu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ili kuwalinda watoto wanapokuwa katika mazingira ya shule. Utaratibu huu unaweza kuanzishwa kwa kupitia kamati za shule.
- Kuangalia upya adhabu ya viboko itolewayo na walimu na kutengeneza mwongozo wa adhabu mbadala kwa walimu kama njia za ufundishaji zisizo na ukatili.
- Kuhakikisha mfumo wa nidhamu kwa walimu wakosaji unaandaliwa.

## Ustawi wa Jamii

Utolewaji wa taarifa chache kuhusu ukatili dhidi ya watoto unasababishwa na mambo mengi. Watoto wengi na walezi hawajui waende wapi kupata huduma. Majaribio ya kuzifikia huduma mara nyingi hukwamishwa na vikwazo vya urasimu. Afisa wa Ustawi wa Jamii ni wakala muhimu chini ya Sheria ya Mtoto Na 21 (2009) katika kulinda ulinzi wa mtoto, lakini kuna uwiano usiolingana kati ya uwezo na upatikanaji wa Maafisa wa Ustawi wa Jamii na majukumu yao kwa mujibu wa Sheria.

Hivi sasa, kuna Afisa mmoja wa Ustawi wa Jamii kwa kila watoto zaidi ya 200,000 wa Kitanzania. Matokeo ya utafiti huu, pamoja na nia iliyoelezwa ndani ya sheria ya mtoto, inatoa wito wa kuboresha Idara ya Ustawi wa Jamii na

kuongezwa kwa kiwango kikubwa idadi ya Maafisa wa Ustawi wa Jamii. Baada ya kuongeza idadi ya Maafisa wa Ustawi wa Jamii, Idara ya Ustawi wa Jamii itahitaji msaada mkubwa wa kuwajengea uwezo maafisa hawa ili kuwa na kikosi chenye ujuzi na uwezo, kwa miaka ijayo. Maafisa hawa watakuwa ndio wa kupokea watoto waathiriwa na kuwasaidia katika mfumo wa rufaa, na baadae kusimamia kurejeshwa katika makazi salama na shuleni, mara baada ya uchunguzi wa polisi na maswala ya huduma za afya kukamilika.

Njia ya mawasiliano kwa ajili ya msaada wa mtoto (Child Helpline) itatoa fursa ya kuimarisha namna ya mtoto atakavyoweza kutoa ripoti na kuondoa tatizo la kiwango kikubwa cha kutotolewa taarifa kama ilivyoonyeshwa na utafiti huu.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inaongoza juhudi za serikali za kuanzisha njia hiyo ya mawasiliano. Nambari ya kupiga simu bure iliyosajiliwa ni -116. Rasilimali watu na fedha zitahitajika ili kuhakikisha kuwa mfumo huo wa mawasiliano unaandaliwa vizuri na kuwajengea uwezo watumishi na kuwafuatilia ili kutoa huduma yenye manufaa. Ikishakuwepo, njia hii ya mawasiliano itawapa watoto wanaohitaji matunzo na ulinzi njia ya mawasiliano ya moja kwa moja, na pia itakuwa ni chanzo kikubwa cha habari juu ya unyanyasaji katika ngazi ya familia na jamii ambazo zitakuwa ni muhimu kwa waandaaji wa mipango na utekelezaji wa sera.

**Hatua zinazopendekezwa:**

- Kusaidia kuboresha rasilimali watu na kuwajengea uwezo ili kuongeza wingi na ubora wa watumishi wa ustawi wa jamii katika Jamhuri ya Tanzania.
- Kuimarisha jukumu kuu la Idara ya Ustawi wa Jamii pamoja na watumishi wake wanaoongezeka ili kuwa wakala mkuu wa ulinzi wa watoto na msimamizi wa Mfumo madhubuti wa rufaa wa Ulinzi wa Watoto.
- Kuendeleza ushirikiano kati ya Idara ya Ustawi wa Jamii na sekta za haki, afya, elimu na jumuiya za kiraia ili kuhakikisha kuwa kazi ya rufaa dhidi ya ukatili kwa watoto inafanywa kwa wakati na kwa namna yenye kuleta matokeo.
- Kukamilisha utayarishaji wa sheria na muongozo inayotokana na Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 Na 21 (2009), ambayo inatafsiri vipengele vya Sheria hiyo kwenye taratibu zitakazojumuisha sekta mbali-mbali katika kukabiliana na unyanyasaji na ukatili dhidi ya watoto, ambao zitachangia katika mfumo wa kitaifa wa kulinda watoto.
- Kuandaa mfumo wa taarifa zinazohusiana na ulinzi kwa watoto ambao utakuwa na usimamizi na tathmini ya kufuatilia jinsi kesi za ukatili dhidi ya watoto zinavyoendesha mpaka maamuzi ya mwisho.
- Kusaidia katika kutengeneza njia ya mawasiliano ya kitaifa (Child Helpline) ya moja kwa moja kwa msaada wa mtoto ili kupata mpango utakaofaa kukabiliana na vitisho, au hata matukio ya ukatili wa kiakili, kimwili au kijinsia dhidi ya watoto.
- Kupanua wigo wa elimu ya malezi na kuwashirikisha watoto katika kuandaa machapisho yenye nadharia chanya, yanayojenga mahusiano yasiyo na ukatili.
- Kushughulikia vikwazo na unyanyapa unaosababisha watoto waliodhalilishwa wasitafute huduma/msaada.
- Kubuni mfumo imara wa jamii wa kutoa tahadhari mapema ili kuwalinda watoto katika maeneo yote ya maisha yao.

## Ubia kati ya Serikali na Jumuiya za Kiraia

Msingi wa mafanikio ya mpango wa kitaifa wa kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto ni kuwepo kwa ubia kati ya Serikali na Mashirika yasiyo ya kiserikali, Asasi za kijamii, kidini na sekta binafsi. Ili kupatikana matokeo yenye kuzaa matunda kwa watoto, ni muhimu juhudi za jumuiya za kiraia zisaidiane na serikali kwa kufanya kazi kwa karibu na kutumia mifumo na taratibu za kitaifa. Utafiti juu ya mtandao wa asasi za kiraia zinazotoa huduma kwa watoto na huduma rafiki zinazomlenga mtoto uliofanywa na Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya ya Sayansi na Tiba cha Muhimbili unatoa taarifa za msingi katika uandaaji wa mpango ya kitaifa wa utoaji huduma.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto itapaswa kuratibu shughuli za watoa huduma za watoto ili kuhakikisha kuwa wanaimarisha mifumo ya serikali, hasa katika ngazi ya jamii ambako ndiko asasi za jamii zimejikita kufanya kazi nchini Tanzania.

Uoanishaji wa sekta ya umma na sekta binafsi kuhusiana na ukatili dhidi ya watoto ni muhimu sana. Matokeo ya ukatili dhidi ya watoto, na kwa kupitia mfumo wa Sheria ya Mtoto Na 21 (2009), kunatoa fursa nyingi za kuimarisha ubia kupitia “Watoto walio hatarini” kwa kulenga zaidi maswala ya unyanyasaji na ukatili ikiwa ni viashirio vya kuwa hatarini – haswa kwenye maswala ya afya.

Ni muhimu mikakati ya kuthibiti ukatili dhidi ya jinsia ijenge mahusiano na Mpango wa watoto walio katika mazingiza hatarishi, mpango wa kuthibiti UKIMWI na Ukatili dhidi ya jinsia, ambapo kutakuwa na ushirikiano katika shughuli za jamii za uhamasishaji wa kubadili tabia ya jamii ya kukubali ukatili wa kijinsia. Ni muhimu mbinu za kuelimisha jamii zitumike kama njia ya kuzuia ukatili kwa kuwashirikisha wanawake, wanaume na watoto kujua ukatili haukubaliki na kuwaelimisha athari za ukatili haswa zile za kiafya.

Kikundi kazi cha Kumlinda Mtoto, chini ya mpango wa Kundi la Wabia wa Utekelezaji la Watoto walio katika mazingira hatarishi, litahitaji kupanuliwa ili kujumuisha wabia wengi zaidi ikiwa ni sehemu ya mdahalo wa kitaifa unaoendelea hivi sasa ili kulileta suala la ulinzi wa mtoto katika *Mpango wa Taifa wa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi uliofanyiwa makisio kwa mwaka (2011- 2015).*

**Hatua zinazopendekezwa:**

- Kuunga mkono Jukwaa la Haki za Mtoto Tanzania katika kutengeneza mwongozo wa namna ya *kuendesha Uhamasishaji na Utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Na 21 (2009): Mwongozo kwa Asasi za Kijamii*
- Kujenga mfumo wa kitaifa na wa baina ya wizara kusaidia uhamasisha katika mambo yanayohusiana na ulinzi wa mtoto, pamoja na ukatili dhidi ya watoto kuwa shughuli kuu muhimu katika *Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Watoto walio katika mazingira hatarishi uliofanyiwa makisio kwa (2011- 2015)*.
- Kuandaa majukumu madhubuti ya kusaidiana Serikali na wafadhili na shughuli zao zinazohusiana na kumlinda mtoto na hasa katika kushughulikia ukatili dhidi ya watoto.

## Utoaji huduma wa serikali za mitaa

Kufuatana na Sera ya madaraka kwenda ngazi za chini, jukumu na wajibu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, chini ya ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa litakuwa ndiyo muhimili mkuu utakaoamua uratibu na utekelezaji wa huduma muhimu kwa watoto kwenye sekta zote, na wadau wote.

Uwezo wa Serikali ya Tanzania wa kupeleka madaraka ngazi ya chini kuhusiana na fedha na rasilimali watu litakuwa ni jambo muhimu litakaloleta mafanikio ya utaratibu wa kudumu wa kumlinda mtoto katika ngazi ya Wilaya na ngazi za chini za utawala. Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI itakuwa na jukumu muhimu katika mchakato huu kwa kuhakikisha kuwa Maafisa wa Ustawi wa Jamii wanasambazwa na fedha za kutosha kwa uwiano wa idadi ya watoto wanaohitaji matunzo na huduma za ulinzi zinatolewa.

## Uzinduaji wa kampeni ya kuhamasisha jamii kutokomeza ukatili dhidi ya watoto

Matokeo ya utafiti wa *Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania*, jukumu la Kikosi Kazi kinachojumuisha Sekta mbalimbali na jinsi Serikali inavyopanga kutekeleza na kuzuia ukatili dhidi ya watoto nchini Tanzania, kunahitaji mikakati madhubuti ya mawasiliano katika ngazi mbalimbali – ikiwa ni pamoja na kutumia vyombo vya habari vya aina mbalimbali katika kusambaza ujumbe katika jamii na asasi mbalimbali kuhusiana na kuwalinda watoto.

Kuandaa ujumbe wenye kuleta maana kwa muktadha wa jamii ya Tanzania, kwa kuzingatia desturi zilizopo, huku ukishinikiza kuwepo kwa desturi zenye mtazamo wa kuwalinda watoto, itakuwa ndiyo kazi endelevu ya Serikali na wadau wa sekta binafsi. Japokuwa matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa ukatili dhidi ya watoto nchini Tanzania ni wa kiwango cha juu, hii haina maana kuwa kutoa ujumbe unaolaani ukatili huu unakubalika, bali kutumia fursa hii kushinikiza kuwepo kwa mabadiliko ya uhakika ya kuwalinda watoto wanaoishi katika jamii iliyo katika mfumo wa mabadiliko ya kasi.

Kubadilisha mwenendo wa kijamii na vigezo hatarishi vinavyotoa mwanya wa ukatili dhidi ya watoto kuwa ujumbe wenye kuleta matokeo yanayofaa na unaoambatanishwa na uzuiaji na utoaji huduma za kuwalinda watoto, itakuwa ndiyo lengo kuu kwa miaka mingi ijayo.

## Wajumbe wa kikosi kazi kinachojumuisha Sekta mbalimbali

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto (WMJJW)

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (WHVUM)

Wizara ya Kazi na Ajira

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (WAUJ)

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (WEMU)

Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba (WSMK)

Wizara ya Mambo ya Ndani (WMN)

Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OW-TAMISEMI)

Shirika la Taifa la Takwimu

Tume ya UKIMWI Tanzania (TACAIDS)

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya ya Sayansi na Tiba cha Muhimbili

Shirika la Afya Duniani (WHO)

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA)

Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UNWOMEN)

Shirika la Umoja wa Mataifa la UKIMWI (UNAIDS)

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF)

Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM)

Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID)

Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, Ofisi ya Tanzania (CDC Tanzania)

PACT

Save the Children

Picha ya jalada: UNICEF/Julie Pudlowski

Kwa taarifa zaidi wasiliana na mratibu wa Ripoti ya Ukatili dhidi ya Watoto Tanzania, UNICEF, S.L.B 4076,
Dar es Salaam, Tanzania au kupitia barua pepe: daressalaam@unicef.org


WALINDE